
## CHANZO KIKUU CHA MAJI YA KUNYWA

Asilimia 51 ya kaya Tanzania zinatumia maji ya bomba kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa.

**Asilimia ya Kaya Zinazotumia Maji ya Bomba kama Chanzo Kikuu cha Maji ya Kunywa kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## MATUMIZI YA VYOO

Asilimia 60 ya kaya Tanzania, asilimia 59 Tanzania Bara na asilimia 90 Tanzania Zanzibar zinatumia vyoo vilivyoboreshwa.

## VYANZO VYA NISHATI YA KUPIKIA NA KUANGAZIA

- Asilimia 56 ya kaya Tanzania zinatumia kuni na asilimia 26 zinatumia mkaa kwa ajili ya kupikia.
- Asilimia 37 ya kaya Tanzania zinatumia umeme wa gridi ya Taifa kwa ajili ya kuangazia.

## OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU

**Dira**

Kuwa kitovu cha takwimu rasmi Tanzania

**Dhima**

Kutoa takwimu rasmi zilizo bora na huduma zinazokidhi mahitaji ya wadau wa Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya kupanga mipango na kufanya maamuzi yenye uthibitisho

**Mawasiliano**

Mtakwimu Mkuu wa Seriksli,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
64 Barabara ya Lusinde; S.L.P 2683; 41104 Tambukareli;
Dodoma - Tanzania.
Simu: +255(0)26 2963822, Fax: +255(0)26 2963828
Barua pepe: sg@nbs.go.tz, Tovuti: www.nbs.go.tz

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

**Dira**

Kuwa kituo cha ubora kwa uzalishaji wa takwimu na kukuza utamaduni wa sera na kufanya maamuzi kulingana na ushahidi

**Dhima**

Kuratibu uzalishaji wa takwimu rasmi, kutoa takwimu za hali ya juu na taarifa na kukuza matumizi yake katika kupanga, kufanya maamuzi, utawala, ufuatiliaji na tathmini

**Mawasiliano**

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar,
S.L.P 2321, Zanzibar.
Simu: +255(0)24 2231869, Fax: +255(0)24 2231742
Barua pepe: zanstat@zanlink.go.tz, Tovuti:
www.ocgs.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

MATOKEO YA SENSA YA SITA
TANZANIA
SENSA
2022
MIPANGO JUMUISHI KWA MAENDELEO ENDELEVU

## MATOKEO MUHIMU KUTOKA KWENYE RIPOTI YA TAKWIMU ZA MSINGI ZA KIDEMOGRAFIA, KIJAMII NA KIUCHUMI

# MATOKEO MUHIMU KUTOKA KWENYE RIPOTI YA TAKWIMU ZA MSINGI ZA KIDEMOGRAFIA, KIJAMII NA KIUCHUMI – SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022; TANZANIA

## IDADI YA WATU

Tanzania ina idadi ya watu 61,741,120 (wanaume 30,053,130 na wanawake 31,687,990); Tanzania Bara ina idadi ya watu 59,851,347 (wanaume 29,137,638 na wanawake 30,713,709) na kwa upande wa Tanzania Zanzibar kuna jumla ya watu 1,889,773 (wanaume 915,492 na wanawake 974,281).Sehemu kubwa ya watu Tanzania (asilimia 65.1) wanaishi maeneo ya vijijini na asilimia 34.9 wanaishi maeneo ya mjini.

## MUUNDO WA IDADI YA WATU KIUMRI

Asilimia 49 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 18 na asilimia 3.8 wana umri wa miaka 65 na zaidi, hivyo Tanzania kuna watoto wengi zaidi ikilinganishwa na watu wazima.Uwiano wa umri tegemezi kwa Tanzania na Tanzania Bara ni watu 87 kwa kila watu 100 wenye umri wa nguvu kazi na kwa Tanzania Zanzibar ni watu 78.

## MUUNDO WA KAYA

Wastani wa idadi ya watu katika kaya Tanzania ni watu 4.3, kwa vijijini ni watu 4.6 na kwa mjini ni watu 3.8.

Wastani wa idadi ya watu kwa kila kaya katika kaya zinazoongozwa na wanaume ni 4.4 na 4.0 katika kaya zinazoongozwa na wanawake.

## HALI MPYA YA NDOA

Wastani wa Umri wa kuingia kwenye ndoa kwa mara ya kwanza nchini Tanzania ni miaka 24. Wanawake ni wastani wa umri wa miaka 22 na wanaume miaka 26.


## NYARAKA ZA UTAMBULISHO WA KITAIFA NA URAIA

Asilimia 47 ya watoto chini ya miaka mitano wana cheti cha kuzaliwa. Takriban asilimia 7 ya watu nchini Tanzania wana bima ya afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) au Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHIF).

## UMILIKI WA ARDHI

Takriban asilimia 11 ya wanawake nchini Tanzania wanamiliki ardhi binafsi ikilinganishwa na asilimia 18 ya wanaume.

**Piramidi ya Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri; Tanzania, SWM 2022**




## UMILIKI WA SIMU ZA MIKONONI

Asilimia 85.3 ya kaya Tanzania zina angalau mtu mmoja mwenye umri wa miaka 4 na zaidi anayemiliki simu ya mkononi.


## UTANGULIZI

Kipeperushi hiki kinatoa muhtasari wa matokeo muhimu kutoka kwenye ripoti ya Takwimu za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi kutoka kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Baadhi ya Viashiria vilivyoainishwa ni pamoja na idadi ya watu, vyeti vya kuzaliwa; Uyatima; Elimu; Ulemavu; hali ya makazi na umiliki wa simu za mkononi.

## VYETI VYA KUZALIWA

Asilimia 67.1 ya watu hawana cheti cha kuzaliwa wala tangazo.


**Asiliamia ya Watu Wenye Vyeti vya Kuzaliwa.**




## HALI YA UYATIMA

Asilimia kumi ya watoto chini ya umri wa miaka 18 ni yatima.

**HALI YA UYATIMA TANZANIA SENSA YA MWAKA 2022**





## ELIMU

Kiwango halisi cha uandikishaji (NER) kwa shule za msingi Tanzania ni asilimia 83.3, Tanzania Zanzibar (96.9%) na Tanzania Bara (82.9%).

## IDADI KUSOMA NA KUANDIKA KWA WATU WAZIMA

Asilimia themanini na tatu ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi Tanzania wanajua kusoma na kuandika, Tanzania Zanzibar ni asilimia 90.6 wakati Tanzania Bara ni asilimia 82.8.

**Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima (Miaka 15 na Zaidi) kwa Jinsi; Tanzania, SWM 2022**




## HALI YA ULEMAVU

Kiwango cha ulemavu kwa watu wenye miaka 7 na zaidi ni asilimia 11.2

**Kiwango cha Ulemavu kwa Watu wenye Umri wa Miaka 7 na zaidi kwa Mikoa; Tanzania, SWM 2022**

